




# Miaka 62 ya Uhuru, SUZA yajivunia kuwa sehemu ya ukuzaji taaluma, utafiti na uchumi

Jafari Juma, Mwananchi



Makamu Mkuu wa Chuo cha SUZA, Prof. Mohamed Makame Haji.

Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) ni miongoni mwa vyuo vikuu 19 vilivyopo Tanzania bara na visiwani. Hata hivyo, chuo hiki kina sifa na upekee wake katika kukuza na kuendeleza taaluma visiwani humo huku kikijipambanua katika ubora na tofauti na vyuo vingine.

Chuo hicho kiliazishwa kwa sheria namba nane ya mwaka 1999 ambayo ilifanyiwa marekebisho kadhaa, mwaka 2009, 2016, 2019 huku mara ya mwisho ikifanyiwa marekebisho mwaka 2020.

SUZA ikiwa ni taasisi ya elimu ya juu kinayojivunia mafanikio lukuki wakati huu tunapoadhimisha miaka 62 ya Uhuru ikiwemo kuweza kufanya tafiti ambazo zinasaidia jamii na Serikali kwenye kupanga mipango mbalimbali ya kimaendeleo.

SUZA kimekuwa ni sehemu ya kusaidia ajenda kuu ya Serikali ya ukuzaji wa Uchumi wa Buluu kwa kuzalisha wahitimu waliobobea kwenye masuala ya utalii, kilimo, Kompyuta, ujasiriamali na TEHAMA.

Aidha, kupitia taaluma za fani hizo, wanafunzi na wanataaluma wanaandaa miradi mbalimbali ya kusaidia ukuaji wa uchumi wa buluu kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali na jamii kwa ujumla.

Kwa upande wa sekta ya mawasiliano na utamaduni, SUZA kwa sasa kimekuwa ni kielezo kikuu cha ukuzaji na utangazaji wa lugha ya Kiswahili ndani na nje ya nchi kwa njia za kutoa elimu, kuandaa mijadala na makongamano, kutumia kazi za sanaa na mbinu nyingine.

Aidha, chuo kimekuwa kikipata ushirikiano kutoka vyuo mbalimbali duniani ambapo kwa njia moja ama nyingine inasaidia kukitangaza nje ya mipaka ya Tanzania na hii imetokana na Uhuru na mahusiano mazuri na nchi nyengine.

Katika kufikia kujenga Taifa lenye watu walioelimika na kutambua fursa mbalimbali zilizopo ndani na nje ya Zanzibar, SUZA kimeweka mikakati mbalimbali. Miongoni mwa mikakati hiyo ni;

Kuandaa warsha, semina, makongamano na kuwaalika watu wenye fani mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa ajili ya wanafunzi na wanataaluma kwa lengo la kujifunza mambo mbalimbali pamoja na kuwapatia mbinu za kutumia fursa zilizopo ndani nan je ya chi.

Chuo kinatekeleza miradi ambayo kwenye utekelezaji wake wananchi wanapata fursa moja kwa moja ya kushiriki na kujifunza mambo mbalimbali kwa mujibu wa maeneo ya mradi husika. Miradi inayotekelezwa na SUZA imeleta manufaa makubwa kwa chuo na nchi kwa ujumla. Miongoni mwa miradi hiyo ni;

Mradi wa HEET unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, umeanza kutekelezwa kwenye kipindi uongozi wa Dk Samia Suluhu Hassan wenye lengo la kuimarisha elimu ya juhu nchi na kuchangia mageuzi ya kiuchumi. Mradi umetoa fursa kwa zaidi ya watumishi 50 kuenda masomoni ndani na nje ya nchi kwenye ngazi ya Shahada ya Uzamili na Uzamivu hadi sasa.

Mradi wa BSU ambao unafadhiliwa na DANIDA, SUZA kimeshiriki kwenye mradi huu kuanzia awamu ya kwanza mpaka ya tatu ambayo imemalizika mwaka huu na tayari kimepata nafasi ya kuendelea kwenye awamu ya nne.

Kwenye mradi huu SUZA na nchi imefaidika kwa ujumla wake ambapo kuna wafanyakazi wamepata nafasi za ufadhili wa masomo ya muda mfupi na mrefu, ununuzi wa vifaa vya maabara za Sayansi (maabara ya kemia) chuo kimepata vifaa vya kisasa vinavyoweza kutumiwa na wanafunzi wa shahada ya Uzamili na Uzamivu kwa ajili ya tafiti mbalimbali.

Mradi wa DALILA wenye lengo la kutumia utaalamu kwa upatikananji wa nishati mbadala mbali na nishati ya umeme wa maji pamoja na kufungua fursa za kiuchumi.

Mradi wa GeoICT4e unaojihusisha na masuala ya mtengamono baina ya jografia na tekinolojia ya mawasiliano (ICT) kwa kufanya tafiti na kuandaa mbinu mbalimbali za kitaaluma na ubunifu kwa wataalamu wetu, wanafunzi na jamii ya watanzania kwa ujumla.

Mradi huu unatekelezwa na vyuo vikuu vitano vya Tanzania ambavyo ni SUZA, UDSM, MOCU, Nelson Mandela na ARU na kwa upande mwengine Chuo Kikuu cha Turku cha nchini Finland.

Chuo kinatoa elimu kwa makundi mbalimbali kupitia Skuli yake ya Kilimo ambayo imekuwa ikifanya programu za kuwafikia wakulima waliopo Pemba na Unguja kupitia mradi wa TANRICE kwa kuwapatia elimu na njia ya kilimo cha mpunga na mazao mengine.

SUZA kama ilivyo vyuo vikuu vyengine Afrika inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa majengo, wanataaluma vifaa na kuzidiwa na mahitaji ya wadau na wanafunzi wanotaka kujiunga, Chuo kimeandaa mpango mkuu wa upanuzi ambao unatarajiwa kutekelezwa kwa miaka ishirini kwa awamu tatu tofauti.

Mpango huu utawezesha kuimarisha miondombinu ya majengo na vifaa, kuongeza idadi ya watumishi wenye sifa na vigezo vinavyohitajika, kuongeza idadi ya program za kitaaluma nk.

CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)
*Kichocheo cha Mabadiliko ya Jamii*

SALAMU ZA PONGEZI ZA KUTIMIZA MIAKA 62 UHURU:
9 DISEMBA, 1961 – 9 DISEMBA, 2023

Baraza la Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kwa niaba ya Menejimenti ya Chuo na Wanajamii wote wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), linatoa salamu za pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa wananchi wote wa Tanzania kwa kuadhimisha miaka 62 ya Uhuru wa Tanganyika. Aidha Chuo kinajumuika na Watanzania wote katika kusherehekea siku hii adhimu.

Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kinafarijika kupokea miongozo kwa ajili ya uimarishaji wa elimu ya juu na kinaahidi kuendeleza juhudi za kutimiza wajibu wake wa kuchangia maendeleo ya elimu nchini na kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii kupitia utoaji wa elimu bora.

***Miaka 62 ya Uhuru, Amani na Umoja ni nguzo ya Maendeleo yetu***

Kwa taarifa zaidi kuhusu Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar tembelea tovuti
http:// www.suza.ac.tz
Mawasiliano yote rasmi na Chuo yafanywe kupitia kwa:
Makamu Mkuu wa Chuo
Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar
Sanduku la Posta 146
Zanzibar, Tanzania
Barua pepe: vc@suza.ac.tz

